# HADITHI FUPI: UTANZU ULIOPUUZWA

*E.S. Mohochi*

## Utangulizi

Fasihi imegawika katika makundi mawili, kundi la kwanza ni la fasihi simulizi ambayo kimsingi huhifadhiwa kwa njia ya masimulizi na la pili ni la fasihi andishi inayohifadhiwa kwa njia ya maandishi. Kila kundi limegawika zaidi katika tanzu mbalimbali, kila mmoja ukiwa na kaida na taratibu zinazoupambanua na kuutofautisha na mwingine. Makala haya yatajihusisha na hadithi fupi ambayo ni moja kati ya tanzu za fasihi andishi. Katika makala haya, nitaonyesha kwamba utanzu wa hadithi fupi haujapewa umuhimu unaostahili, hasa tunapoulinganisha na tanzu nyingine za fasihi andishi zikiwemo riwaya, tamthilia na ushairi.

Jamii nyingine zimekuwa na hadithi fupi katika tamaduni zao tangu enzi na enzi, kwanza katika masimulizi ya mdomo na hatimaye katika maandishi. Ngano ndiyo aina ya fasihi iliyofuata wimbo wa kazi na ushairi katika jamii (Senkoro 1982; Msokile 1992). Wengine wanaoshikilia msimamo kwamba hadithi ni kazi ya fasihi ambayo ina historia ndefu sana katika jamii ni pamoja na: Carpenter na Neumeyer (1974), Allen (1981), De Grandsaigne (1985), Mphahlele (1986) na Lohafer na Clarey (1989).

Hadithi zimekuwa sehemu ya utamaduni wa jamii nyingi ulimwenguni zikisimuliwa miongoni mwa wawindaji, baina ya wanawake nyumbani wanapotekeleza shughuli zao za kila siku, katika vyumba vya watoto na hata madarasani katika viwango mbalimbali vya elimu. Muda huo wote watu walisimuliana hadithi kwa madhumuni ya kuburudishana, kutoleana mafunzo mbalimbali na pia katika tamasha na sherehe tofautitofauti.

Katika enzi ya masimulizi hadithi fupi zilijitokeza katika miundo na mitindo mbalimbali. Awali, hadithi nyingi za mapokeo (ngano) zilitumia wahusika wanyama kueleza hali ya maisha ya binadamu. Hatimaye, hadithi hizi zikaanza kutumia mchanganyiko wa wahusika wanyama na binadamu. Kuibuka kwa maandishi kulipoashiria njia nyingine ya kuwasilisha kazi za sanaa, hadithi vilevile iliathiriwa kutokana na mabadiliko katika uwasilishaji. Mjadala wa makala haya utajikita zaidi katika hadithi fupi za kubuni ambazo ni sehemu ya fasihi andishi.

## Kupuuzwa Kwa Hadithi Fupi

Japo hadithi fupi zimekuwa sehemu ya utamaduni wa jamii nyingi kwa muda mrefu, ni suala la kusikitisha sana kutambua kwamba hadithi fupi zimepuuzwa katika taaluma ya fasihi, hasa katika uwanja wa uhakiki. Baada ya kuibuka na kushamiri katika jamii mbalimbali, hadithi zimekumbana na

misukosuko kadha wa kadha ambayo ilichangia hali ya kupuuzwa kwake. Ferguson (katika Whafer na Clare, 1989:176) anaeleza hali hii kwa kusema hivi:

> Kama ilivyo katika jamii ya watu, kuna mvutano katika matabaka ya fasihi. Baadhi hujitahidi kupanda ngazi ya hadhi huku mengine yakijikuta yanazidi kudidimia na hata kupotea kabisa. Watu wa tabaka la juu walikuwa na fasihi pevu, ambayo ilidaiwa, haingefurahiwa na wanyonge. Wachochole kwa upande wao, wakajikita katika fasihi pendwa iliyowaliwaza na kuwapa matumaini huku hadithi fupi ikiwa mojawapo ya kazi ya sanaa zilizotekeleza wajibu huo kwa muda mrefu (tafsiri yangu).

Dondoo hili linadokeza hali ya mvutano na ukinzano katika matabaka ya watu katika jamii huku baadhi yakidai kumiliki tanzu maalum za fasihi. Katika misingi hiyo, si ajabu kwamba hadithi fupi ilipuuzwa kwani ilinasibishwa na wanyonge ambao ilidaiwa walikosa uwezo wa kuifurahia aina nyingine ya fasihi. Msimamo kama huu unaitazama hadithi kama kazi duni inapolinganishwa na kazi nyingine, jambo ambalo si la kweli kwani halina msingi wowote wa kitaaluma. Hata hivyo, hali hiyo iliyozikumba jamii za kimagharibi haikujitokeza wazi katika jamii nyingi barani Afrika. Katika jamii nyingi barani Afrika, mgawanyo kama huo wa matabaka, huku baadhi yakidai kumiliki fasihi maalum haukuwepo. Ndipo sasa tunaona kuwa hadithi fupi hazikudunishwa katika misingi hiyo ya kutengewa watu wa tabaka fulani. Kwa mfano, katika fasihi ya Kiswahili, hakuna madai thabiti yoyote ya kuonyesha kuwa hadithi fupi zilidunishwa na kutazamwa kama kazi ya wanyonge.

Wengi walizidharau kutokana na ufupi wake wakidai kwamba ilishughulikia suala mojamoja peke yake hivyo ikawa pungufu kisanaa. Baina ya karne ya 15 na 17 utanzu wa hadithi fupi, kwa sababu ya kupuuzwa, ulididimia zaidi. Sababu nyingine ni kwamba wakati huo tenzi na kazi za kitanzia ndizo kazi za sanaa zilizokuwa muhimu miongoni mwa watawala. Katika karne ya 18 na 19 hadithi fupi zilianza kuchapishwa kwa wingi magazetini na katika majarida mbalimbali ili iweze kuwavutia watu wengi. Kwa mfano, Allen (1981) anaitaja hadithi ya "*The two Drovers*" ya Walter Scott iliyochapishwa kwenye *Chronicles of Canongate*, 1827, kuwa hadithi ya kwanza ya kisasa katika Kiingereza. Huko Marekani, mwaka wa 1837, Hawthorn akaandika *Twice Told Tales*. Licha ya juhudi hizo, hadhira kubwa ya wasomi ilipendelea riwaya. Katika miaka ya nusu ya pili ya karne ya 19 hadithi zilichapishwa vitabuni, kama fasihi ya watoto pamoja na kazi nyingine.

Kufikia miaka 1870, hadithi ilifaulu kujisimamia kidete kando ya riwaya. Hali hii ilimaanisha kuwa, kinyume na awali, hadithi fupi iliweza kuchapishwa vitabuni kama kazi inayojitegemea bila ulazima wowote wa kuchapishwa pamoja na kazi nyingine yoyote. Katika fasihi ya Kiswahili, hadithi za kwanza

kuchapishwa vitabuni zilikuwa za kimapokeo. Mifano ni pamoja na; *Hekaya za Abunuwas na Hadithi Nyingine*, kilichochapishwa mara ya kwanza 1935, na *Hadithi za Bibi* (1970).

Pamoja na ukweli kwamba kurunzi ya uhakiki ulianza kuiangaza hadithi fupi katika miaka hiyo, hali hii ilidorora sana. McClave (1980) anasikitika kuwa kufikia wakati huo hadithi fupi zilikuwa hazijapewa umuhimu kiakademia kama vile ushairi, insha, tamthilia au riwaya. Anawasihi wahakiki zaidi kujihusisha na hadithi fupi kwani kuna upungufu mkubwa sana kwa tahakiki katika utanzu huu.

Hali sawa na hiyo iliikumba hadithi fupi hapa barani Afrika na Dlamin (1988), anasema kuwa uchunguzi wake wa hadithi fupi za Kiafrika umetokana na ukosefu wa uhakiki wa hadithi hizo. Tukiigeukia fasihi ya Kiswahili, tunakuta hali ya kusikitisha zaidi. Hadi sasa ninafahamu tahakiki tatu tu za hadithi fupi za Kiswahili. Kuna uhakiki wa *Uwike Usiwike Kutakucha* uliofanywa na Senkoro na Mollel katika *Mulika* Na. 15, 1983. Wahakiki hawa waligusia kimuhtasari tu, masuala muhimu ambayo Ruhumbika aliyashughulikia katika kila moja kati ya hadithi nne za diwani hiyo. Zaidi ya hayo, walieleza namna ambayo mwandishi ametumia mbinu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile ngano ili kuyaeleza maudhui ya wakati wake katika "Dua la Kuku Lilivyompata Mwewe". Tahakiki ya pili ni ile ya Alphonse Kabano ambaye alichunguza ujenzi wa wahusika katika hadithi za "Nyoka Hana Mjomba" ya W.A. Macha na "Mwanamke Mzuri" ya J. Katondo zilizomo katika *Parapanda* (Ruhumbika 1982). Tahakiki yake inapatikana katika jarida la *Mwanga: Sauti ya Chuo Kikuu cha Rwanda* Na. 8, 1988. Kama vile Mollel na Senkoro, Kabano hakuzama sana katika uhakiki wake (Mohochi, 1995).

**Sababu za Kupuuzwa**

Kuna sababu kadhaa ambazo zilitinga ustawi wa uendelezaji wa hadithi fupi kama utanzu wa fasihi. Sababu hizo ndizo zimechangia hali ya hadithi fupi hivi sasa katika fasihi pamoja na jamii kwa jumla. Hebu sasa tuchunguze sababu hizo moja baada ya nyingine.

***Hadhira***

Kwanza kabisa, kuna swala la hadhira ama wasomaji. Tumekwishaona kwamba kwa muda mrefu hadithi fupi ilitambwa kama sanaa ya wachochole katika jamii za kimagharibi. Watu wa matabaka ya juu walipendelea kazi walizoziona pevu zaidi. Idadi ya wasomi ilipoongezeka, watu wengi zaidi wakapendelea kusoma kazi ndefu. Kisha kukawa na ustawi wa viwanda na uvumbuzi wa vifaa vya kupiga chapa ambavyo vilifanikisha uchapishaji wa riwaya na kazi nyingine ndefu.

Katika hali hiyo, tunaona kuwa hadithi fupi andishi haikuwa na hadhira pana sana ya wasomaji. Shaw (1983) anatudokezea kuwa hadithi ilichelewa kupata umaarufu kwingineko (hasa Uingereza) kama ilivyokuwa Marekani na Ufaransa kwani, katika miaka ya kwanza ya karne ya kumi na tisa Waingereza walikuwa wamebobea katika usomaji wa riwaya.

Inawezekana pia kuwa watu wengi hawakuzitilia maanani hadithi fupi kwa sababu tumekuwa nazo tokea zamani katika mazingira mbalimbali. Hili linaweza kueleza hali ya hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili kwani inawezekana kuwa watu hawakuipapatikia kama walivyozipapatikia kazi mpya zilizoibuka kama vile riwaya. Binadamu ana mazoea ya kufurahia na kupendelea vitu vipya kwani kipya kinyemi ingawa kidonda. Kwa hivyo, ukosefu wa idadi kubwa ya watu wenye hamu ya kuzisoma likawa pigo kubwa sana kwa hadithi fupi.

## *Mfumo wa Elimu*

Kimsingi, tunapojadili mfumo wa elimu tunalimulika suala pana la ukosefu wa wasomaji japo kwa kuzingatia kundi maalum la hadhira ya fasihi katika jamii. Katika jamii ambazo watu hawajajenga mazoea na mwenendo wa kusoma kazi mbalimbali za fasihi kwa madhumuni ya kujistarehesha, shule huwa ni chemichemi ya hadhira kubwa sana ya wasomaji. Ndipo basi, hapa Afrika Mashariki riwaya, tamthilia na ushairi husomwa zaidi mashuleni na vyuoni kwani ni sehemu muhimu ya masomo katika viwango mbalimbali vya elimu.

Kwa bahati mbaya, mifumo ya elimu katika mataifa haya, ambayo imejengeka katika misingi ya kimagharibi ilizingatia zaidi riwaya na kupuuza hadithi fupi katika maandishi ya nathari. Kwa hivyo, walimu wanafundisha yale yaliyo muhimu wakiwatayarisha wanafunzi kwa mitihani yao na kupuuza utanzu wa hadithi fupi ambao hautahiniwi.

Mfumo mpya wa 8-4-4 umeleta mageuzi kidogo kwa sababu hivi sasa hadithi fupi ni somo la lazima katika mfumo huu (Tindyebwa, 1988). Hata hivyo, hali hii haibainiki katika fasihi ya Kiswahili, hasa katika ngazi ya elimu ya sekondari. Hadithi fupi ni sehemu muhimu sana ya fasihi andishi ya Kiswahili na hakuna sababu inayoridhisha ya kutoifanya sehemu ya fasihi ya Kiswahili inayofundishwa na kutahiniwa katika shule za upili, kama ilivyo katika fasihi ya Kiingereza.

Jambo la kutia matumaini kidogo ni kwamba baadhi ya vyuo vikuu hapa nchini vimeanza kuipatia hadithi fupi nafasi katika masomo yao, kama vile Chuo Kikuu cha Nairobi, Chuo Kikuu cha Moi, Chuo Kikuu cha Maseno na Chuo cha Nairobi kule Kikuyu. Katika Chuo Kikuu cha Egerton, kwa muda mrefu, hadithi fupi imekuwa kijisehemu tu cha kozi nzima ya maandishi ya nathari katika fasihi ya Kiswahili. Hivi sasa kuna kozi nzima ya hadithi fupi inayofunzwa katika

mwaka wa tatu kama kozi ya hiari. Aidha, hadithi fupi hufunzwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama sehemu ya kozi pana ya maandishi ya kubuni (*creative writing*). Bila shaka hali kama hii ikiendelea idadi ya wasomaji wa hadithi fupi itaongezeka.

***Wahakiki***

Wahakiki wana nafasi muhimu sana katika uendelezaji wa kazi yoyote ya fasihi. Kwa kiwango fulani, wao huwa daraja baina ya mwandishi na idadi kubwa ya wasomaji. Wahakiki huwafaa pia waandishi kwa kutaja makosa yanayojitokeza katika kazi zao. Baadhi ya wahikiki husukumwa na manufaa ya kifedha wanayotarajia na iwapo hakuna hadhira iliyo tayari kuzinunua na kuzitumia tahakiki zao, ni wachache sana watakoendelea kuziandika. Hali hii ya ukosefu wa hadhira inaweza kueleza ukosefu wa tahakiki za hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili kwani kama tulivyotaja, kufikia hivi sasa tumeona tatu tu: ya Senkoro na Mollel (1983), ya Kabano (1988) na ile ya Mohochi (1995).

Kundi hili hujaribu kuyakinisha madai yao kwa kusema kuwa waandishi walioandika hadithi fupi katika miaka ya 1970 kama Ngugi wa Thiong'o, Kibera na Taban waliacha na kuingilia kazi nyingine za fasihi. Hata hivyo, inawezekana kwamba waliuacha uandishi wa hadithi fupi kwa sababu nyingine kabisa kama vile: uandishi wa hadithi kuwawia mgumu, ukosefu wa soko kwa sababu wasomaji na wachapishaji hawazipendelei. Msimamao kama huo miongoni mwa wahakiki ni kikwazo kikubwa sana kwa uendelezaji wa hadithi fupi. Iwapo wanaamini kwamba hadithi fupi ni kazi duni na hata waandishi kadhaa waliacha kuziandika, ni wazi kwamba hawatazitilia maanani. Matokeo ya hatua hiyo yatakuwa kuyakosa manufaa ya uhakiki katika taaluma ya hadithi fupi. Tunaamini kuwa hadithi fupi zikipewa nafasi muhimu katika mfumo wa elimu, wahakiki nao vilevile wataziangaza zaidi.

***Waandishi***

Waandishi pia wanaweza kupigwa mafungu. Kuna wale wanaoandika kwa sababu wanaongozwa na msukumo wa mahitaji ya pesa tu, waandishi wanataaluma ya fasihi, pamoja na wale wanaoandika kwa msukumo wa hamu na karaha. Mwandishi katika mojawapo ya makundi hayo hawezi kuwafikia wasomaji bila kupitia kwa wachapishaji. Iwapo hadithi hazichapishwi, waandishi watakwama hata kama wameandika vizuri kiasi gani. Tatizo la uchapishaji limewafanya waandishi wengi wa hadithi fupi kuelemea zaidi upande wa magazeti. Katika hali kama hiyo, waandishi wanaoandika kwa minajili ya mauzo wataacha kushughulikia hadithi fupi kwani hazichapishwi na kununuliwa kwa wingi.

Aidha, kwa mujibu wa De Grandsaigne (1985) mtambaji wa ngano alishikilia nafasi muhimu sana katika jamii ya kijadi ilhali mwandishi wa hadithi fupi hadi sasa hajatambuliwa vilivyo wala kupata sifa kutoka kwa wahakiki na jamii kwa jumla. Kuna baadhi ya waandishi wa hadithi katika fasihi ya Kiswahili ambao huandika pia kazi nyingine wala si hadithi fupi tu. Kwa mfano Mohammed S. Mohammed, E. Kezilahabi, M. Mulokozi na wengineo. Waandishi hawa wanatambulika na kufahamika zaidi kutokana na maandishi yao mengine wala si kwa hadithi fupi walizoziandika. Kwa hivyo, waandishi wa hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili hawajatambuliwa kiasi cha kutosha kuwachochea kuandika zaidi na kuwatamanisha wengine kujiunga nao. Hili linawezekana iwapo kazi zao zitachapishwa na kusomwa kwa wingi zaidi. Ikitokea hivyo, watapata jina na motisha wa kuandika kazi zaidi.

### *Wachapishaji*

Ama kwa hakika wachapishaji ni wafanyabiashara. Ni nadra sana kwao kuchapisha kazi kwa sababu wanataka kukuza taaluma fulani bila kujali mauzo yanayotarajiwa. Wachapishaji ni kiungo muhimu sana kati ya waandishi na wahakiki kwa upande mmoja na hadhira inayolengwa. Kwa upande mwingine, mashirika mbalimbali ya uchapishaji yanaweza kusaidia au kuwa kikwazo kikubwa sana katika ustawi wa kazi ya sanaa za uandishi. Mchango wa uchapishaji katika uendelezaji wa kazi yoyote ya sanaa ni muhimu sana kwa sababu kimsingi, makundi yote tuliyoyataja kuhusu kupuuzwa kwa hadithi fupi hutegemeana na kuwasiliana kutokana na uchapishaji.

Kwa muda mrefu sana, utanzu wa hadithi fupi za Kiswahili umekumbwa na matatizo kutoka kwa wachapishaji. E. Kezilahabi na M. Mulokozi ni baadhi ya wasanii waliowahi kuandika miswada ya hadithi ambayo haijatufikia kwani haikuchapishwa kwa hofu kuwa huenda isipate wateja wa kutosha. Haya ndiyo yanayoelezwa na Shaw (1983) anaposema kwamba, wachapishaji walikuwa tayari kuchapisha kazi ndefu kama riwaya kuliko hadithi fupi na sababu kubwa ya hali hii ilikuwa ukubwa wa hadhira iliyokuwa na hamu ya kusoma kazi hizo.

Kuna vitabu vingi vya hadithi fupi vinavyochapishwa kwa Kiingereza na Mcmillan Publishers kwa madhumuni ya kutumiwa kama vifaa vya kuendeleza wanafunzi katika Kiingereza. Katika fasihi ya Kiswahili, awali kulikuwa na mfululizo wa vitabu kwa ushirikiano wa Longman na British Broadcasting Corporation. Vitabu hivi havichapishwi tena. Labda ni kwa sababu mahitaji hayajitokezi waziwazi katika hadithi fupi za Kiswahili kwa sababu hazifundishwi mashuleni.

**Hitimisho**

Kutokana na yale yaliyojadiliwa katika makala haya ni wazi kwamba hadithi fupi hazijashughulikiwa vya kutosha kama tanzu nyingine za fasihi andishi. Nimeonyesha jinsi ambavyo makundi kadhaa katika jamii yamechangia hali hiyo. Ninaamini kuwa hali hii inapaswa kubadilika kwani hadithi fupi si duni na zina nafasi muhimu sana katika jamii sambamba na kazi nyingine za fasihi.

Jambo la kutumainisha kwa wapenzi wa hadithi fupi ni ukweli kuwa licha ya pingamizi hizo zote, hadithi zinaendelea kushikilia nafasi muhimu sana katika fasihi. Japo zimepuuzwa katika ngazi ya uchapishaji wa vitabu na tahakiki, zimeendelea kuwa maarufu sana miongoni mwa wasomaji wa kawaida kuliko ilivyo riwaya. Kinyume na riwaya, hadithi fupi hupatikana katika magazeti ya kila wiki na zinaweza kuwafikia wengi.

Nikiongea juu ya mifumo ya elimu nchini Kenya na Tanzania nimebainisha kuwa kuna matumaini ya hadithi fupi kupanda ngazi zaidi na zaidi. Ama kwa hakika katika fasihi ya Kiswahili kinachozidumaza zaidi hadithi fupi si ukosefu wa wasomaji au uchapishaji wa vitabu ama magazeti bali ni ukosefu wa kazi mbalimbali za kiuhakiki na kinadharia kuhusu hadithi fupi za Kiswahili.

Ninashikilia msimamo sawa na wa Lohafer (Lohafer na Clarey, 1989) kuwa hadithi fupi zinaendelea na zitaendelea kupigania nafasi yake muhimu. Anasema kuwa utanzu huu unazidi kupata umaarufu miongoni mwa maprofesa na wachambuzi wa fasihi kwa jumla.

Kwa vile ufupi wake haujawa sababu ya kutotimiza majukumu kadha wa kadha yanayotekelezwa na kazi nyingine za fasihi, hakuna sababu mathubuti ya kuendelea kuzipuuza. Wakati umefika ambapo wahusika wote wa fasihi ya Kiswahili wazinduke na kuzipa hadithi fupi nafasi muhimu zinayostahili katika fasihi ya Kiswahili na Kiafrika kwa jumla.

## Marejeo

Allen, w. (1981) *The Short Story in English*. New York: Oxford University Press.

Dlamin, F.L. (1988) *The Short Story in Africa: Its History and Criticism* Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mclave, H. (1980) (Mhariri) *Women Writers of the Short Story*, Prentice - Hall, Inc.

Mohochi, E.S. (1995) *Fani katika Hadithi Fupi ya Kiswahili*. Tasnifu ya M.A., E.U.

Mphahlele, E. (1986) *A Guide to Creative Writing*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Msokile, M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Ruhumbika, G. (1978) "Dua la kuku lilivyompata mwewe", katika *Uwike Usiwike Kutakucha*. Dar es Salaam: Eastern Africa Publications.

-------------- (Mhariri) (1982) *Parapanda*. Arusha: East African Publications Limited.

Senkoro, F.E.M.K. na Mollel, J. (1983), Tahakiki ya *Uwike Usiwike Kutakucha*, katika Mulika, Na.15, Dar es Salaam: TUKI.

Shaw, V. (1983) *The Short Story: A Central Introduction*. New York: Longman Inc.

Tindyebwa, G. (1988) *A Guide to Chameleon's Second Delivery*. Nairobi: Stellagraphics Ltd.